HOTUBA YA UKARIBISHO ILIYOTOLEWA NA FELIX G. KIBODYA RAIS WA CHAMA CHA WANASHERIA TANZANIA BARA (TANGANYIKA LAW SOCIETY) KWENYE MKUTANO MKUU WA MWAKA WA CHAMA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 19 FEBRUARI 2011 KWENYE UKUMBI WA AICCC ARUSHA

Mhe. Mizengo Kayanza Pinda, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Celina Kombani Waziri wa Katiba na Sheria

Wah. Viongozi waalikwa

Wanasheria wenzangu,

Mabibi na Mabwana.

Mhe. Waziri Mkuu,

Awali ya yote, kwa niaba ya Baraza la Uongozi (yaani Governing Council) la chama cha wanasheria Tanzania Bara (TLS) ningependa kuchukua fursa hii kutoa shukrani zetu za dhati kwa kukubali kwako kujumuika nasi leo hii kwenye Mkutano wetu wa Mwaka. Sote tunafahamu fika kuwa umeacha majukumu mengi ya kitaifa. Na tunatambua kuwa umetokea Dodoma ambako, hadi jana jioni ulikuwa unasimamia shughuli za serikali bungeni.

Kuwepo kawko pamoja nasi leo hii ni ishara maridhawa ya imani yako wewe binafsi na serikali yetu kwa chama chetu na wanachama wake.

Pili napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuteuliwa kwako na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadaye kuthibitishwa na Bunge letu Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania. Kuteuliwa kwako tena kunadhihirisha imani aliyo nayo Mhe. Rais katika utendaji wako na haswa katika taaluma yetu yasheria.

Tatu, nachukua fursa hii kuto rambirambi za wanachama wetu kutokana na kadhia ya mabomu yaliyolipuka Gongola Mbota jijini Dar es Salaam na ambayo yamesababababisha vifo na majeraha kwa watu pamoja na uharibifu mkubwa wa mali. Tunawatakia wahanga wa janga hili la kitaifa wapiti afueni ya haraka.

Mhe. Waziri Mkuu,

Chama cha wanasheria Tanzania bara kilianzishawa takriban miongo sita iliyo pita. Kwa kifupi kina umri wa mtu aliyefikia muda wa kustaafu kazi kwa lazima! Kwa maana hiyo hiyo basi, chama chetu ni kikongwe. Pamoja na umri huo mkubwa, chama chetu kina majukumu na wajibu mkubwa sio kwa wanachama wake bali kwa jamii ya watanzania. Moja kati ya majukumu yetu ni kuhakikisha kuwepo kwa utawala wa sheria na utawala bora.

Jamii ya wanasheria wanaounda jumuiya ya chama inafikia wanachama 1,700 katika daftari la wanasheria yaani Roll of Advocates. Idadi hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwepo kwa shule ya sheria yaani the Law School of Tanzania pamoja na mikakati madhubuti iliyobuniwa na Mheshimiwa Jaji Mkuu wa kuwasaili kwa haraka zaidi waombaji (petitioners). Tunataraji kuwa idadi ya mawakili itaendelea kukua ili kuleta uwiano unaokubalika wa mwanasheria mmoja na watu anaopaswa kuwahudumia.

Hivyo basi, nadiriki kusema, jamii ya wanasheria niliyoitaja hivi punde ndiyo yenye jukumu la kuhakikisha kuwa watanzania wote bila kujali kipato, wana haki iliyo sawa mbele ya sheria. Je, jukumu hili linatekelezeka? Nadhani jibu la swali hili siyo rahisi. Sisi kama chama, tunajitahidi sana kadri ya uwezo wetu kutoa msaada wa sheria kwa wananchi wasi na kipato cha kuwawezesha kugharamikia ada za wakili.

Mhe. Waziri Mkuu,

TLS kupitia kamati yake ya msaada wa sheria (yaani legal assistance committee) imekuwa ikitoa msaada wa sheria kwa kuwasikiliza waombaji wenye matatizo ya kisheria na pale inapostahiki, kufungua mashauri mahakamani. Zaidi ya hayo, kuanzia mwaka 2017, TLS iliazimia kutenga siku moja kila mwka kuwa siku ya msaada wa sheria. Mwaka jana, siku hiyo iliazimishwa Mwezi Novemba katika mikoa kumi ya Tanzania bara. Kitaifa, siku hiyo iliazimishwa huko Dodoma ambapo mgeni rasmi alikuwa Mhe. Celina Kombani (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria. Hapa napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza serikali kwa kutoa ufadhili wa sikiu ya sheria kila mwaka kupitia Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria yaani Legal Sector Reform Program.

Hata hivyo si budi nikiri kuwa, pamoja na kuweko kwa juhudi hizi, safari bado ni ndefu. Hapa nachelea kutamka kuwa mchango wa serikali unahitajika tena kwa kasi kubwa zaidi. Wote tunafahamu kuwa upatikanaji wa haki ni haki ya Msingi ya binadamu inayotamkwa pia katika Katiba yetu. Lakini haki hiyo itapwelea kama haiwezi kutekelezwa kwa kiasi cha kuridhisha.

Kwa maantiki hiyo tunataraji kuwa serikali itakamilisha kwa haraka mchakato wa kubuni na hatimaye kupitisha sera ya msaada wa sheria na baadae kuitungia sheria. Kama mdao wa karibu, TLS iko tayari kutoa mchango wake ili kutimiza azma hii muhimu.

Mhe. Waziri Mkuu,

Jana tulikuwa na mdahalo wa kihistoria uliozungumzia katiba ya nchi yetu. Chama kiliwaalika watoa mada toka sehemu mbalimbali barani Afrika hususan Afrika Mashariki. Mdahalo huu umeibua hoja nyingi tena za Msingi ambazo kwa maoni yangu zitaisaidia serikali katika mchakato unaohusu mstababali wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jana Jioni nilitoa Taarifa ya awali kwa vyombo vya habari kuhusiana na maswala muhimu yaliyojadiliwa.

Sote tunafahamu fika kuwa mjadala wa katiba ni wa kitaifa na utachukua sura ya pekee baada ya kupitishwa kwa mswaada wa sheria unaotarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwezi Aprili mwaka huu. Kwa maantiki hiyo, chama chetu kimedhamiria kuchukua nafasi ya mbele (yaani lead role) katika jambo hili muhimu kwa taifa letu. Hivyo basi, napenda kukutaarifu kuwa Taarifa ya majadiliano haya yatawasilishwa katika ngazi husika pale muda utakapojiri ili yaweze kufanyiwa kazi.

Mhe Waziri Mkuu,

Yako mengi ya kujifunza, yako mengi ya kufanya pia yako mengi ya kuyaweka kando. Kama alivyotuasa Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Nyerere, alisema Kupanga ni Kuchagua. Kama chama, tumebuni Mpango Mkakati (yaani Strategic Plan) unaolenga utekelezaji majumu yetu ya msingi. Moja kati ya malengo yetu ni kujenga kituo chetu cha kutoa msaada wa sheria yaani Legal Aid and Advocacy Centre. Tumekwisha nunua eneo, tumekamilisha upembiuzi yakinifu wa kutekeleza mradi. Tumefanya maaamuzi magumu ya kumtaka kila mwanachama wetu kuchangia sh. 50,000 kila mwaka kwa ajili ya LAAC. Ni rai yangu kwa serikali kuziona juhudi hizi chini ya mwavuli wa msaada wa sheria kwa umma na kuangalia uwezekano wa kuchangia sehemu ya gharama za ujenzi wa jengo hili.

Mhe. Waziri Mkuu,

Baada ya kusema haya machache, napenda sasa, kwa niaba ya mawakili wa Tanzania bara waliopo mbele yako, kukukaribisha ili utoe Hotuba yako ya Ufunguzi wa Mkutano wetu wa Mwaka 2011.

Karibu sana, Mhe. Waziri Mkuu!